

[Draft for Dissemination]

**KATIBA YA CHAMA CHA WAMILIKI
WA DHAMANA TANZANIA (TASH)**

**CONSTITUTION OF THE TANZANIA
ASSOCIATION OF SECURITIES HOLDERS
(TASH)**

October, 2009

**KATIBA YA CHAMA CHA
WAMILIKI WA DHAMANA
TANZANIA (TASH)**

YALIYOMO

KAULI YA UTANGULIZI							(ii)
SEHEMU							UKURASA
I	UANZISHWAJI WA CHAMA	1
II	UFAFANUZI	1-2
III	MALENGO NA MAJUKUMU YA CHAMA	2-4
IV	UANACHAMA	4-6
V	DAFTARI LA WANACHAMA	6-7
VI	KUKOMA UANACHAMA	7
VII	KIINGILIO, ADA YA KILA MWAKA NA HAKI ZA MWANACHAMA	7-8
VIII	NGAZI ZA CHAMA NA UONGOZI	8-11
IX	MAMLAKA NA MAJUKUMU YA VIONGOZI NA WATENDAJI WA CHAMA	11-14
X	MASHARTI YA UCHAGUZI WA VIONGOZI NA MUDA WA KUSHIKA MADARAKA	14
XI	VIKAO VYA CHAMA	15
XII	MASUALA YA FEDHA	15-17
XIII	WADHAMINI WA CHAMA	17-18
XIV	MAREKEBISHO NA MABADILIKO YA IBARA ZA KATIBA	18-19
XV	MIGOGORO YA UWEKEZAJI	19-20
XVI	TAREHE YA KUENZA KUTUMIKA	20
XVII	MLEZI..	20
XVIII	KUVUNJA CHAMA	20
 <u>MAJEDWALI</u>							
	JEDWALI LA KWANZA	21
	JEDWALI LA PILI	22

KAULI YA UTANGULIZI

SISI wamiliki wa dhamana Tanzania tuliojumuika kwenye Mkutano Mkuu wa Tatu wa Mwaka wa Uwekezaji wa Mfuko wa Umoja uliofanyika tarehe 6 Desemba, 2008 katika Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam,

TUKIWA NA ARI ya kuunda chombo imara cha kutuunganisha katika utetezi wa maslahi yetu, kwa maendeleo yetu kiuchumi na maendeleo ya masoko ya mitaji katika nchi yetu,

TUKIAFIKI kwamba masharti chini ya Sehemu ya 1 ya Ibara ya 3 ya Katiba ya dhamana ya Uwekezaji Tanzania yanatuunganisha pamoja kuwa washiriki muhimu wa Meneja pamoja na wadau wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania,

TUKITAMBUA fursa na mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyopo nchini kwetu hivi sasa katika azma ya kufikia malengo yetu na kuwahamasisha wananchi wengine katika masoko ya mitaji ,

TUKIJUA NA KUAMINI kwamba umoja ni nguzo muhimu katika kukuza na kuharakisha kasi ya kuyafikia malengo tarajiwa,

HIVYO BASI, TUMEAMUA KUUNDA Chombo cha Umoja wetu, yaani “CHAMA CHA WAMILIKI WA DHAMANA TANZANIA” kwa madhumuni ya kukuza na kulinda maslahi ya wenye dhamana waliopo sasa na watarajiwa nchini Tanzania pamoja na kushiriki katika kuhamasisha wananchi ili washiriki kwenye masoko ya mitaji.